# *Sema Na Mwamba Nao Utatoa Maji Yake*

Asante, ndugu.

2 Mnaweza kuketi. Samahani kwa kuwaweka mkisimama huku mkiimba kwa muda mrefu sana, lakini ndiyo kwanza nikutane na rafiki wa zamani ambaye sijamwona kwa miaka mingi, papa hapa nje, Ndugu Noel Jones. Tulikuwa tukiwinda pamoja huko Arkansas. Mlinisikia nikizungumzia jambo hilo mara nyingi, yule jamaa aliyekuwa na macho ya mjusi, ambaye angeweza kuwapiga risasi kuchakulo mahali ambapo hata nisingeweza kuwaona. Na kwa hiyo, ilitokea tu kwamba nilimtambua, alibadilika kidogo, naye ni babu sasa, lakini hakika nilifurahi kumwona.

3 Mtu fulani aliniambia, mmoja nanii wangu, katibu wangu wa mikutano ya nje, kwamba—kwamba—kwamba kuna rafiki yangu mwingine hapa usiku wa leo, rafiki wa zamani, Ndugu Morrison kutoka huko chini karibu—huko chini karibu na San Francisco. Sijui kama Ndugu Morrison angesimama, ama kuinua mkono wake, ama chochote kile, ambapo ningeweza . . . [Ndugu fulani anasema, "Morris."—Mh.] Morris, Ndugu Morris. Ubarikiwe. Hakika nina furaha kukuona tena. Mungu akubariki.

4 Loo, maskini mwalimu wa Biblia. Ninakumbuka . . . Hivi huyo ndiye dada, pamoja nawe hapo? Naam, vema, hakika nina furaha ku—kuwaona. Bwana awabariki. Walikuwa baadhi ya wadhamini wangu wa kwanza nilipokuja Pwani ya Magharibi kwa mara ya kwanza miaka mingi, mingi iliyopita. Loo, hili liligeuka likawa juma la kurudi nyumbani, sivyo? Ajabu!

5 Vema, tuna furaha kuwa na ndugu yetu na dada, na Ndugu Jones, Dada Jones. Nami ninakumbuka yapata miaka hiyo iliyopita, sidhani bado yuko ndani, yuko huko nyuma akizungumza na baadhi yao, sisi . . . aliniuliza, nilikuwa yapata siku nane mchana na usiku mimbarani, akasema, "Ndugu Branham, hivi hupendi kuwinda kidogo tu?"

Nikasema, "Loo, ninapenda."

6 Akasema, "Vema, nitakupeleka mawindoni," nami na Ndugu Johnson. Kwa hiyo alikuwa na bunduki ya marisau ya kale ya 97, ninyi watu mnajua ninalozungumzia, bora kuliko zote zilizowahi kutengenezwa. Halafu basi, kwa hiyo basi alikuwa na maskini bunduki nyingine pale ambayo walikuwa wameazima, ambayo ilikuwa tu ile ya kale ya kusukuma, mwajua, ile—ile bunduki ya kale. Na kila wakati ungerusha risasi moja, ingefungua ninii . . .

inakubidi kuwa na kijiti, kuisukuma risasi kutoka nyuma. Ndipo Ndugu Noel akaniambia, akasema, "Sasa, Ndugu Branham, wewe chukua bunduki *hii*."

Nikasema, "La, ninaweza kukushinda siku yoyote kwa *hii* hapa."

Akasema, "Nakwambia, afadhali uchukue hii bunduki."

7 Kwa hiyo wakamfungulia huyo mbwa, naye akawafukuza kuchakulo kumi na watano wakapanda juu ya mti, ndipo akabweka. Tukaanza kukimbia mahali alipokuwa, akasema, "Sasa, kama unataka kuchakulo, hii ndiyo nafasi yako ya mwisho, afadhali uchukue bunduki hii."

Nikasema, "Endelea tu kusonga mbele."

8 Vema, jamaa huyo alikuwa na kama kuchakulo watatu wakitoroka, sijawahi kuona upigaji risasi mwingi namna hiyo maishani mwangu, kuchakulo wakianguka kila mahali. Nilipiga risasi mara moja, kitu hicho cha kale karibu kiniangushe chini, ni—nilikuwa nikijaribu kusukuma ganda kutoka kwake.

9 Tulimchukua Ndugu Johnson siku chache baadaye, huyo alikuwa ni baba mkwe wake, nasi ilitubidi kutembea kupitia kwenye—kwenye, mbuga ndogo ya vinamasi, kama ilivyo, huko mbali Arkansas kule. Naye, kwa hiyo alikuwa na jozi moja ya buti. Kwa hiyo, Ndugu Noel alikuwa ndiye mkubwa kuliko wote, mrefu, jamaa mwembamba, naye akaninyanyua na kuniweka mgongoni mwake, naye huyo akavuka hicho kinamasi. Akarudi na kumchukua Ndugu Johnson, yeye ni maskini jamaa mdogo, mfupi, mnene, akaenda huko nje, nami nikaanza kutania, akaanza kucheka na kumwangusha Ndugu Johnson moja kwa moja katikati ya maji. Loo, jamani!

10 Loo, Mungu ambariki, Ndugu Johnson. Mimi. . .Hivi punde ameniambia kwamba yeye ni mgonjwa sana, kwa hiyo ninaomba ya kwamba Mungu Mwenyezi atamsaidia Ndugu Johnson; huyo ni baba mkwe wake.

11 Loo, nawaambia, popote nilikopitapita, baadhi ya maskini mioyo mizuri sana inadunda chini ya maskini mashati hayo ya kale ya samawati huko Arkansas. Hivi ninyi. . .? Ni Waarkie wangapi waliopo hapa? Hebu tuone mikono yenu. Vema! Wananiambia California yote imejaa Waokie na Waarkie, kwa hiyo. . .Vema, hilo ni sawa kabisa. Watu wazuri sana huko Oklahoma na Arkansas pia. Kwa kweli, kila mahali unapokutana na watu wa Mungu, wao ni watu wazuri, sawa kabisa, kila mahali.

12 Tulikuwa na mkutano mzuri sana asubuhi ya leo, ushirika mzuri kwenye kiamshakinywa cha Wafanyabiashara wa Full Gospel. Nilifika kule nimechelewa kidogo, lakini nikapata kufurahia baadhi ya baraka za Bwana. Bwana alishuka na kutubariki nilipokuwa nikizungumza juu ya *Njia Iliyowekwa Na*

*Mungu Ya Ushirika*, na jinsi ambavyo Mungu alituona kupitia Damu ya Mwanawe, nazo dhambi zetu nyekundu zilikuwa nyeupe kama theluji.

13 Sasa, kesho usiku, shukrani kwa yeyote yule, aliyebadilisha ibada hiyo kutoka alasiri mpaka usiku, kwa sababu bila shaka . . . niliiombea. Sasa, hatutaki kujaribu kuondoa mikutano kutoka makanisani, tunajaribu kufanya mikutano yetu namna hii alasiri ili watu waweze kuhudhuria makanisa katika, kwenye, kwenye ibada zao wenyewe. Lakini ingekuwa joto kali sana ungalifanywa kesho alasiri. Na kwa hiyo tuna furaha sana kwamba wahudumu wanayafungua makanisa yao, na kadhalika, kuja mkutanoni.

14 Sasa, ninyi wageni hapa, asubuhi jitafutieni moja ya makanisa haya mazuri hapa bo—bondeni mhudhurie, popote utakapoona kanisa zuri, kanisa ulilochagua. Hawa wahudumu, nadhani tayari wametambulishwa, na kadhalika, na kuambiwa wanakotoka, hudhurieni baadhi ya makanisa hayo asubuhi, na halafu, na kuwasaidia, kwa sababu wanaachilia ibada zao, wengi wao, kesho usiku kuhudhuria ninii, ibada hii hapa.

15 Mungu awabariki, ndugu zangu, hilo ni jambo la kishujaa, huo ni ushirikiano mzuri, ninauthamini. Ni mambo kama hayo, ambayo huleta moyoni mwa mtu, ambayo yanamfanya atake kurudi tena, kwa namna fulani, kuwa na ushirika. Ninatumaini ya kwamba kutakuwako na watu watakaookoka, kwamba makanisa yenu yatafanikiwa. Na shauku yoyote uliyo nayo moyoni mwako, Mungu na akujalie, ninyi, na ninyi watu wazuri ambao mumetupatia ushirikiano huu mzuri katika siku hizi zenye joto za uamsho huu.

16 Kesho alasiri, tunakusudia . . . Niliahidi ya kwamba kila mtu anayekuja mkutanoni atapata kadi ya maombi, tuna siku kadhaa za upambanuzi, tunajaribu kuokota hizo kadi baadaye, halafu kila mtu aliyehudhuria, aliyetaka kadi ya maombi, angeweza kupata moja, nami ningemwombea kila mtu aliyekuwa na kadi ya maombi, kila mtu aliyetaka kuombewa, hakika ningemwombea. Kwa hiyo tutajaribu kufanya hivyo usiku wa leo na kesho alasiri, ama, kesho usiku.

17 Kadi zitatolewa yapata saa moja kabla ya ibada. Ningesema kama ikianza saa moja na nusu, saa kumi na mbili na nusu. Wote wanaotaka kadi ya maombi, njoni saa kumi na mbili na nusu mkaichukue. Sababu ya sisi kufanya hivyo, ni vema sana kwao kuja upesi wawezavyo kuchukua kadi, lakini tunatoa nafasi kidogo pale kwa sababu hatutaki kukatiza ibada zingine.

18 Katibu wa hudumani, Ndugu Goad, Ndugu Mercier, na hao wengine ndio kwanza wanitangazie, kwamba bila shaka, kesho itakuwa imechelewa sana kupata kanda ama vitabu. Tumeifanya kuwa tabia ya kutouza kamwe Jumapili, hasa sana kanda hizi, na vitabu, na chochote walicho nacho. Sasa, vitu hivyo si mali

yangu, si vyangu. Sipati pesa zozote, ninapata mshahara kutoka kwa kanisa langu, dola mia moja kwa juma.

19 Na kwa hiyo, kama tungeweza tu kupanda mbio kwenye barabara kuu ya kwenda Mbinguni namna hiyo, si tungekuwa tukifanya jambo fulani? Kama hizo mbio za mkweche zinazoendelea huko nje; lakini siamini wanaweza kunizamisha, siamini wanaweza, tunaweza tu kupiga makelele tuzizamishe. Kama kuta za Yeriko zilianguka kwa kupiga makelele, mbona, kidogo haingedhuru sasa, sivyo? Labda pingu zingeanguka basi.

20 Kwa hiyo tunatazamia usiku wa kesho uwe usiku mkuu. Na sasa, ninii. . . Kama nilivyosema, ninapata mshahara kutoka kwa kanisa langu, dola mia moja kwa juma, na pesa zingine zote ambazo haziko kwenye kampeni, zinaingia kwenye wakfu, halafu zinawekwa kando ili zisiwe zangu, wala mtu mwingine yeyote, zinatumika kwa ajili ya misheni za kigeni. Ninapokusanya pesa za kutosha pamoja, ambapo ninaweza kwenda ng'ambo, ninaenda kuwahubiria makafiri, hao ambao hata hawajui Yesu ni Nani. Na mle ndani tumeona matokeo yaliyo makuu sana, mikutano yetu iliyo mikubwa sana.

21 Huko Durban, Afrika Kusini, niliona wenyeji elfu thelathini wanaovaa blanketi wakimpokea Yesu Kristo kama Mwokozi binafsi katika wito mmoja wa madhabahuni, elfu thelathini. Bombay, India, kwa Waislamu, na hao wengine, ilikuwa ni vigumu kusema, hakuna njia ya kuwahesabu. Ilikadiriwa humo mjini kuhudhuria mikutano, watu laki tano. Hata tusingeweza kuwaweka popote, wengi mno hata ilinibidi kuondoka kwa sababu tusingeweza kupata mahali pa kutosha kuwaweka. Tunatarajia kurudi hivi karibuni, ambapo tutapanda kwenda mpaka New Delhi, ambako ra—rais alitupa uwanja mduara ambamo tunaweza kuweka watu milioni moja, uwanja mduara wa nje, mandhari ya milimani. Tunatarajia mambo makuu kule.

22 Na kule kwa wale watu wasiojua, maskini wavulana weusi wanaosimama namna hiyo, kamwe hawajapata kuoga maishani mwao, hawajui mkono wa kulia na wa kushoto ni upi, wangesimama huku maskini machozi yao yakitiririka mashavuni mwao kusikia wakati mmoja pekee hadithi ya Mungu anayewapenda. Unapofanya hivyo, rafiki yangu. . . Ninajua tunayasaidia makanisa yetu hapa nyumbani, hiyo ni kweli kabisa. Lakini hapa ambapo tuna makanisa makubwa kwenye kila kona, minara-pia mizuri, mikubwa, mirefu, na kila kitu, na maskini jamaa hao wadogo, Yesu alikufa kwa ajili yao kama tu vile alivyomfia mtoto wako na mtoto wangu.

23 Yeye ana njaa vivyo hivyo, anashikwa na njaa tu kama watoto wetu wafanyavyo, na si haki kwamba tuna kila kitu, hata tuna madoido, nao maskini jamaa hao wadogo hawakusikia Injili hata mara moja. Nafikiri ni wajibu wetu kuipeleka. Na

kama hamwezi kufanya hivyo, sadaka mnazotoa, katika sadaka ya upendo kwangu, ninawatakeni mjue ya kwamba . . . Sijui . . .

24 Endapo hakuna gharama za kulipiwa, sichukui sadaka ya upendo. Na kama matumizi hayajalipiwa, sina budi kuagizia na kukopa hizo pesa, mimi mwenyewe, kulipia matumizi. Kamwe hatuondoki mjini tukidaiwa hata senti moja, hiyo ndiyo rekodi yangu. Na kama ikifikia mahali ambapo Mungu haidhamini mikutano yangu, wala ha—haijilipii, basi wakati wangu wa kuja nyumbani umewadia, kuichunga maskani tena.

25 Sijawahi kuchukua sadaka maishani mwangu, daima nimemtegemea Mungu. Kamwe katika uamsho wangu nisingewaruhusu watu kuombaomba, kudoeza, na kushawishi. Kama watu wanampenda Mungu, watu maskini, wata—wataunga mkono yote wawezayo, na kama hawawezi, basi itanibidi kufanya hivyo, nitazikopa kwa njia nyingine, kutoka kwa rafiki yangu, ama chochote kile, nipate kuulipia.

26 Halafu basi mimi, kama wameulipia wote, kisha ni huru, nipewe sadaka ya upendo, hata siiangalii, katibu wangu huichukua, na kuitayarisha, nayo inawekwa benki, na kuiweka benki chini ya jina la Maskani ya Branham huko New Albany, Indiana, na huko pesa hizo haziwezi kutumiwa kwa kitu kingine chochote, bali kwa ajili ya Ufalme wa Mungu, kuzisadia misheni za kigeni ninapoenda huko kuhubiri. Ndipo basi ninapoweka akiba ya kutosha mle ndani kwenda, basi ninaondoka na kwenda. Sasa, ninaamini hiyo ni kuwafanya tu watu wajue jambo hilo, kwamba ni nini.

27 Vitabu hivi tulivyo navyo, ni vya Ndugu Gordon Lindsay, ni vyake, yeye huviandika. Tunavinunua kutoka kwake kwa asilimia arobaini kuliko vile anavyoviuza. Wavulana hawa wanalipwa kuuza vitabu hivi, wanalipwa kuvisafirisha. Vingi vyake vinapotea, vingi vinasambazwa bure, daima hatupati faida kwenye vitabu.

28 Hao wavulana wanauza kanda kwa ajili ya maskani. Sasa, kanda hizo ni bidhaa zenye hatimiliki, na hazina budi kuwekwa kwenye kanda iliyo bora sana. Kama vile hivi vitabu, kama haviridhishi, virudisheni, mpate kurudishiwa pesa zenu. Mnaona? Sisi . . . Nazo ka—kanda zinauzwa kwa bei rahisi sana. Santuri, na chochote unachonunua, si zangu, ni za wengine, tunaziweka tu mkutanoni.

29 Na kama sikufikiri haingewasaidia, ama kuisadia huduma, hakika nisingeruhusu ziuzwe. Nami ninaichunguza, nione kama kuna shida yoyote na bei, nazilinganisha na zingine, na kama kuna kitu chochote kinachoonekana kuuzwa ghali mno, papo hapo, ningekomesha hilo sasa hivi. Naam, bwana. Sina hilo.

30 Lakini usiku wa leo, ukitaka vitabu, ama kadhalika, *Hadithi Ya Maisha Yangu*, *Nabii Azuru Afrika*, mahubiri, *Mfano Wa Tai Ataharikishavyo Kiota Chake*, *Je, Unaogopa Kansa*, vingi vya

hivyo vingine, *Yesu Kristo, Yeye Yule Jana, Leo, na Hata Milele*, *Sikuliasi Ono La Mbinguni*, vingi vya vitabu hivyo, ukitaka, santuri, kanda, unaweza kuzipata mwishoni mwa jengo hapa, mahali fulani. Ni wapi hapo, Gene? Huko nyuma? Kuna ridhaa ya vitabu, nadhani, huko nyuma kwamba mnaweza kuvipata usiku wa leo pekee, kwa kuwa kesho hatutaviuza.

31 Sasa, mnaweza kunisikia vizuri, huko nyuma kabisa? Huko nyuma kabisa? Loo, hilo ni sawa. Mimi. . .Hebu mhandisi aipe hii nguvu zote ilizo nazo, mradi tu husababishi uhamishaji.

32 Sasa, unampenda kwa moyo wako wote? Loo, hilo ni sawa tu. Jamani, kwanza kabisa ninajisikia kubarikiwa, usiku wa leo. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

33 . . .tunataka kusoma kutoka katika Kitabu cha Hesabu, kwenu ninyi mnaofuatilia. . .[Sehemu tupu kwenye kanda. Ndugu Branham anasoma Hesabu 20:1-8—Mh.]

> *Ndipo wana wa Israeli, mkutano wote, wakaingia bara ya Sini, katika mwezi wa kwanza, nao hao watu* wakakaa *Kadeshi; naye* (Ngoja kidogo, nina ninii yangu. . .ngoja. . .). . .*mwezi wa kwanza: watu wakakaa Kadeshi; naye Miriamu akafa huko, akazikwa huko.*
>
> *Na hapo hapakuwa na maji kwa ule mkutano: wakajikusanya juu ya Musa na juu ya Haruni.*
>
> *Watu wakashindana na Musa, wakanena, wakisema, Ingalikuwa heri kama tungalikufa wakati ule ndugu zetu walipokufa mbele za BWANA!*
>
> *Mbona mmewaleta kusanyiko la BWANA hata jangwa hili, ili tufe huku, sisi na wanyama wetu?*
>
> *Na mbona mmetupandisha kutoka. . .Misri ili kutuleta* hata *mahali hapa pabaya? si mahali pa mbegu, wala tini, wala mizabibu, wala makomamanga; wala hapana maji ya kunywa.*
>
> *Musa na Haruni* wakatoka *pale palipokuwa mkutano, wakaenda hata mlangoni pa hema ya kukutania, nao. . .wakaanguka kifudifudi: na utukufu wa BWANA ukawatokea.*
>
> *BWANA akanena na Musa, akisema,*
>
> *Twaa ile fimbo, ukawakusanye mkutano, wewe na Haruni ndugu yako, ukauambie mwamba mbele ya macho yao; nao utatoa maji yake, nawe utawatokezea. . .maji katika mwamba: na hivyo. . . utawanywesha maji mkutano na wanyama wao.*

Bwana na aongeze baraka Zake kwenye kusomwa kwa Neno Lake.

34 Na sasa, ninataka kuchukua somo kutoka hapo, Maandiko ya kale yaliingia niani mwangu nilipomwona Ndugu Noel, juu ya u—ujumbe ambao nilikuwa nikizungumzia miaka mingi, mingi iliyopita. Kwa namna fulani nilisahau mengi yake, yale niliyotumia kama muktadha, bali nina hakika Roho Mtakatifu atanifunulia ninapoendelea. Somo langu usiku wa leo ni: *Sema Na Mwamba Nao Utatoa Maji Yake*. . . *Utatoa Maji Yake*. Mnaona, "*Utatoa* maji *Yake*. *Utatoa* maji *Yake*."

35 Hapana shaka ilikuwa ni asubuhi yenye joto, kila mtu alikuwa amechanganyikiwa na kufadhaika, kwa sababu usiku kucha wanyama walikuwa wamelia, na wa—watoto walikuwa wamelia, na watu walikuwa wamezozana, na kubishana, na kugombana.

36 Maskini Musa, ulikuwa ni wakati wa kuogofya sana kwake. Mnaona, alikuwa ameshuka kwenda Misri naye alikuwa amewatoa hao wana kulingana na ahadi ya Mungu naye alikuwa akiwaongoza kwenye nchi ya ahadi, nchi iliyojaa maziwa na asali, pamoja na ahadi ya Mungu kuwalinda, na kuwapa kila kitu walichohitaji, mpaka walipofika kwenye nchi hii tukufu iliyojaa maziwa na asali.

37 Musa, mtumishi aliyeitwa na Mungu, nabii aliyewekwa wakfu, Nguzo ya Moto juu yake, ikimfuata, ikithibitisha maneno aliyosema kwa ishara na maajabu, akienda zake kwenye nchi ya ahadi pamoja na hao wana, mfano wa mfano dhahiri sana, ama mfano, hasa, wa safari ya siku hizi. Tuko njiani kuelekea Nchi ya Ahadi, nasi tunaongozwa na Roho Mtakatifu mkuu. Kama walivyoongozwa katika mambo ya kawaida, tunaongozwa kiroho kwenye Nchi hii kuu ya Ahadi ambayo Mungu alitoa ahadi na kutupa.

38 Mungu alikuwa amewaahidi kuwatimizia mahitaji yao yote, bali nia yao ya kimwili ilikuwa imewatoa katika mapenzi ya Kiungu ya Mungu, na ilikuwa imewapa njia ya jangwani.

39 Hiyo imezidi sana siku hizi, hiyo ndiyo shida ya mengi ya makanisa yetu, wamechukua njia ya kimwili, ya kiakili, na wamekatiliwa mbali, ugavi wa baraka za Mungu za uponyaji na nguvu, na ubatizo wa Roho Mtakatifu, nao wamepitia njia ya jangwani, kwa hiyo tuna mabishano, na ugomvi, na ubishi, na malalamiko. Lakini wale ambao wangali wanadumu katika ile Njia, ni furaha isiyoneneka na iliyojaa utukufu mbele za Mungu, pamoja na Nguzo Yake ya Moto juu yao, pamoja na nguvu, na shangwe, na ishara na maajabu. Jinsi lile Kanisa halisi, lililozaliwa mara ya pili linavyoelekea kwenye Nchi ya Ahadi, ile ahadi ya Uzima wa Milele, Nchi inayobubujika Uzima wa Milele, ambako hakuna maradhi tena, mauti, huzuni, wala chochote cha kudhuru!

40 Sasa, lakini wakati nia za kimwili zilipoanza kuja miongoni mwao, hatimaye ziliwawaondosha kwenye njia kuu wakaingia

jangwani. Walifanya kosa lao baya sana waliposhindwa kuendelea. Walikuwa kwenye safari yao, si maili nyingi sana, wangeweza kufanikiwa katika siku chache pamoja na watu hawa wote milioni mbili huko nje jangwani, kama wangalibaki njiani, lakini walipofika mahali paitwapo Kadeshi-barnea . . .

41 Kadeshi-barnea wakati mmoja, ninaambiwa, ilikuwa ni kiti kikuu cha hukumu. Inasema chemchemi kubwa ama kisima kikubwa pale, visima vingi vidogo, mfano mkamilifu wa Kanisa. Kanisa ndilo kiti cha hukumu, ambapo Mbinguni ni Kiti kikuu cha Hukumu cha Mungu, na vile visima vidogo vinawakilisha makanisa madogo yote huko nje. Nayo hukumu huanza katika nyumba ya Mungu. Mnaona? Hapa ndipo hukumu inapoanzia.

42 Hiyo ndiyo sababu sioni ni kwa nini wengi wanalalamika kwamba mimi huzungumza kwa ukali kupita kiasi, na kujaribu kuwafanya watu wanyooke, na kuwaambia jinsi wanavyoishi, jinsi wanavyovalia, na kuniambia ninaidhuru huduma yangu, wakati kiti cha hukumu ni nyumba ya Mungu. Hiyo ni kweli. *Hapa* ndipo inapoanzia, papa *hapa*, ambapo haki, na uadilifu, na hukumu ya Mungu inapaswa kutoka mimbarani.

43 Sasa, walipofika kule, walipiga kambi. Mungu alikuwa mwema kwao, akawaonyesha maajabu mengi makuu na ishara huko chini Misri. Katika safari yao, Yeye alikuwa amewaandalia kila kitu, lakini hata hivyo iliwabidi kuja mahali hapa ambapo karibu nchi ya ahadi ingeweza kuonekana, muda kidogo tu baada ya wao kuondoka. Basi walipofika mahali hapa, Musa alichukua mtu kutoka katika kila kabila, na kuwatuma kwenda Kanaani kuipeleleza hiyo nchi.

44 Sote tunaifahamu hadithi hiyo, jinsi walivyofika, wawili kati yao, hadi Yeriko, na jinsi yule kahaba alivyokuwa amewaficha wale wapelelezi, na kadhalika, na wote. Walipoingia katika ile nchi, waliipeleleza waone kama wao . . . ahadi hiyo ilikuwa ni kweli. Waliporudi, walileta vichala vya zabibu ambavyo ilichukua watu wawili kubeba kichala kimoja cha zabibu.

45 Mara nyingi nimewazia, kama nchi yenye laana juu yake ingekuza aina hiyo ya zabibu, itakuwaje wakati laana itakapoondolewa? Kitakuwa kichala cha zabibu cha aina gani!, Loo, jamani!

46 Ni—ni—ni—ninapata tu kionjo chake kidogo cha mbele mara moja moja. Nilikuwa nikihubiri hapa si muda mrefu uliopita, nilikuwa nikiwazia asubuhi ya leo, mimi hutoa mate sana, mnajua, nadhani, ninapohubiri, lakini nimekuwa nikila baadhi ya hizo zabibu zilizorudishwa, na kwa namna fulani inanifanya kutoa mate kidogo, mwajua, kama farasi anayekula klova.

47 Kwa hiyo basi wakati sisi . . . Waliporudi, walileta kichala hiki kikubwa cha zabibu, ndipo wote wakakusanyika mbele ya kusanyiko la Bwana, nao wakaleta taarifa, “Loo, Mungu amesema kweli, hiyo nchi imejaa maziwa na asali! Ni nchi nzuri,

ni nchi ya mbegu, itakuza chochote. Loo, ni mahali pazuri sana! Tuna maji mengi na mito na umwagiliaji maji na kila kitu kufanya taifa kubwa."

48 "Lakini loo, Wa—Waamori, na Wahiti, na ninii, wengine wote wako kule, baadhi yao ni majitu, nasi tunaonekana kama panzi wadogo."

49 Basi walipoanza kusema hivyo, loo, nguvu zikawatoka wana wa Israeli. Wakaanza kulia na kupiga mayowe, walikuwa wameondoka Misri wakaja, mambo haya yote, na hayo yalikuwa yametukia.

50 Lakini kulikuwako na wawili, kati ya wale kumi na wawili wote kulikuwa na wawili waliokuwa na ujasiri. Wengine wote walisema, "Hatuwezi, hatuwezi kwenda mbele zaidi, sisi ni... Haiwezekani kwetu kukutana na watu wa namna hiyo."

51 Lakini Kalebu na Yoshua wakasema, "Sisi tunaweza hata na zaidi kuiteka!"

52 Mbona hivyo? Hao wengine, wale wenye sehemu ya kiakili, walikuwa wakiangalia jinsi wale majitu walivyoonekana, lakini Kalebu na Yoshua walikuwa wakiangalia ahadi ambayo Mungu alikuwa ametoa. Sasa, yote yanategemea kile unachoangalia.

53 Kuna watu wanaoketi hapa usiku wa leo waliokuwa kwenye viti vya magurudumu siku moja ama mbili zilizopita usiku, wameamka, wanatembea huku na huku sasa. Inategemea kile unachoangalia, kama ukiangalia mateso yako, kamwe hutaenda mbali zaidi, bali kama ukiangalia ahadi ya Mungu, una haki ya kila baraka ya ukombozi ambayo Mungu aliahidi katika Neno Lake, ni yako. Sawa.

54 Mkristo daima huangalia mambo yasiyoonekana. Kila baraka ya ukombozi ya Mungu ni isiyoonekana. Ninii...Hii hapa silaha yote ya Mkristo: upendo, furaha, imani, uvumilivu, wema, upole, utu wema, subira. Yote ni nguvu zisizoonekana zinazotenda kazi katika moyo wa mwaminio. Amina. Hiyo ni kweli. Tunaangalia vitu tusivyoviona.

55 Kama sisi ni watoto wa Ibrahimu basi hatuenendi kwa kuona, tunaenenda kwa imani, kwa kuwa Ibrahimu alitembea kwa imani na kuviita vitu ambavyo havikuwako kana kwamba vilikuwako, kwa sababu Mungu alisema hivyo.

56 Sasa, Yoshua hakuwa na njia ya kujua angeweza kuuteka mji huo. Kalebu hakuwa na njia ya kujua jambo hilo, lakini hivi ndivyo walivyoliamini: kwa sababu Mungu alisema, "Nimewapa nchi hii. Ninaye Malaika atakayeenda mbele zenu, nanii Wangu...jihadharini msije mkamdharau, kwa sababu Jina Langu liko ndani Yake. Hatawasamehe dhambi zenu, atawararua kupitia me—mekoni, atayatimua manyoya yenu. Ata—atawafanyia mambo. Lakini kumbukeni, mfuateni Yeye,

Yeye atawaongoza kwenye nchi ya ahadi, bali msimdharau, msimkatae, mwaminini Yeye."

57 Sasa, halafu tunaona, na katika safari hiyo, Yoshua alikuwa amegundua kwamba alikuwa amemwona yule Mungu mkuu akiishi pale katika ile Nguzo ya Moto, alikuwa amefanya miujiza ya kila namna, yeye na Kalebu walikuwa wameona hilo, nao walikuwa na matumaini ya kwamba Mungu angetimiza Neno Lake. Mwangalieni Mungu, huko chini Misri, "Nimewapa hiyo nchi, sasa nendeni mkaimiliki."

58 Mungu amempa kila mgonjwa humu ndani uponyaji wa Kiungu, kila mmoja wenu. Yesu alijeruhiwa kwa makosa yetu, kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa. Ni yako, bali itakubidi kupigania kila inchi uliyo nayo. "Kila mahali nyayo za miguu yako ziendapo," Mungu alimwambia Yoshua, "nimekupa wewe." Nyayo za miguu zinamaanisha milki, hebu na tuingie usiku wa leo. Amina. Hebu tuingie. Nyayo za miguu ni umilikaji, hebu na tuchukue kila inchi ya ardhi ambayo Mungu alitupa.

59 Kama huna ubatizo wa Roho Mtakatifu, Petro alisema, "Ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, kwa watu wote walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie." Nyayo za miguu ni umilikaji, hebu twende tukaichukue, ni yetu. "Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele," hebu na tuimiliki. "Kazi nizifanyazo Mimi, ninyi nanyi mtazifanya," hebu tuzimiliki, ni ahadi ya Mungu. Usiangalie hali ya mambo, usiangalie jinsi ilivyo vigumu, hebu tuimiliki hiyo nchi.

60 Tutakuwa na mkutano, kama vile asubuhi ya leo tulivyokuwa na mkutano kule, Roho Mtakatifu akishuka mahali hapo, watu wakipiga mayowe, wakipaza sauti, wakimsifu Bwana, halafu mtu fulani akaja, na kusema, "Niombee, Ndugu Branham." Nikamwekea mikono na kumwombea, nikasema, "Sasa, nenda ukaamini."

61 Sasa, jambo ndilo hili: Ni rahisi kuhisi nguvu za Mungu, kuziona wakati unapoamini, lakini basi inapofikia shindano la kuamua, je, unaweza kumiliki kitu unachokiri kuwa nacho? Jambo ndilo hilo, ndugu. Hatuna budi kuipata, hatuna budi kuichukua, ni yetu, bali utapigania kila inchi.

62 Yoshua alipigania kila inchi ya ardhi kutoka upande mmoja wa nchi hadi mwingine, lakini alikuwa na ahadi, Mungu alisema, "Nimekupa wewe." Amina. Kama kuna majitu, kama kuna wakanamungu, kama kuna makafiri, kama kuna makanisa baridi ya kawaida, inaleta tofauti gani? Mungu alitoa ahadi, hebu tuichukue, ni yetu, ni yetu, ni mali yetu, hebu twende tukaichukue.

63 Usiogope, usibaki nyuma, useme, "Vema, ninaamini siku za miujiza zimepita. Loo, sijui." Usifanye hivyo, huyo haonekani kama mwana wa Ibrahimu. Haidhuru ni umbali gani, ahadi

ilionekana kushikilia, vema, iliendelea kwa muda wa miaka ishirini na mitano, lakini badala ya Ibrahimu kudhoofika, alipata nguvu zaidi wakati wote, kwa kuwa alijua ungekuwa ni mwujiza mkubwa zaidi wakati wote.

64 Nasi tutaombewa usiku mmoja, na kesho yake asubuhi tungali tuna tumbo baya, tutasema, "Labda sikupata uponyaji wangu, sina budi kupitia mstarini tena."

65 Loo, ati unajiita mtoto wa Ibrahimu? Haleluya! Kama Mungu alitoa ahadi, Mungu alitoa ahadi, nawe unaiamini, sijali kinachotukia, ni yako. Pigana na ibilisi kwenye kila sehemu ya ardhi anayosimama, nenda ukaiteke, chukua Upanga wa Neno.

66 Ahadi za Mungu ni za kweli, hakuna kitu kinachoweza kuzizuia, ni ahadi za Mungu. Yeye alitupa ahadi ya hiyo kama tu alivyowapa wana wa Israeli. Kanisa la Kipentekoste limekuja kwenye Kadeshi-barnea yao. Tunaweza? Tunaweza kufanya hivyo? "Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele." Tunaweza kwenda kule juu na kuishika ahadi ya Mungu, na kusema, "Ni kweli, ninaidai, ninaimiliki, ni yangu, Mungu alinipa mimi"?

"Utafanyaje jambo hilo?"

"Sijui, si kazi yangu."

67 Kama vile nilivyokuwa nikihubiri wakati mmoja juu ya Eliya, ndipo mtu fulani akaniambia baada ya ibada, akasema, "Sasa, ngoja kidogo, mhubiri, ninaamini ya kwamba wewe ni mtu mwenye akili timamu kuliko kuamini ati kweli hao kunguru walimletea Eliya samaki na mkate."

Nikasema, "Ninaamini, kila neno lake." Kasema, "Hao samaki walikuwa wamekaangwa na mkate ukaokwa."

68 Akasema, "Ni vipi wewe...? Wapi...? Niambie basi, rafiki yangu," yeye alikuwa ni Shahidi wa Yehova, akasema, "niambie basi, rafiki yangu, hao kunguru walipata wapi samaki waliokaangwa na mkate uliookwa?"

69 Nikasema, "Hilo si juu yangu kuhoji, haikuwa kazi ya Eliya kuhoji, jambo pekee alilojua, aliposhikwa na njaa kunguru walikuwa wameketi pale wakimletea mikate na samaki, naye akala." Nikasema, "Hilo ni jambo lile lile kuhusu ubatizo wa Roho Mtakatifu, siwezi kuwaambia unakotoka, jinsi unavyofika huko, ninajua huo huja, nami huufurahia, hilo tu ndilo ninalojali."

70 Siwezi kuwaambia jinsi uponyaji wa Kiungu unavyofanya kazi. Siwezi kuwaambia jinsi ng'ombe mweusi anavyoweza kula nyasi ya kijani kibichi na kutoa maziwa meupe, bali ninayanywa, kwa vyovyote vile, sijaribu kutafuta fomula yake. Sijui ni kitu gani kinachomfanya Roho Mtakatifu kushuka mkutanoni, na watu kunena kwa lugha na kutabiri, viwete wanaruka kutoka kwenye viti vya magurudumu, na wagonjwa wanaponywa,

siwezi kuwaambia hilo. Jambo pekee nijualo: Mungu ameahidi jambo hilo, na ni mali yetu, hebu tuichukue na tuende nayo. Hawawezi kueleza ni umbali gani kutoka kwa mwezi ama ni molekuli ngapi zilizo katika atomu, hiyo si kazi yao, lakini jambo pekee wanalojua, Mungu aliuahidi, wakaupata na kuufurahia. Amina.

71 Hapo ndipo walipofanyia kosa lao, walipofika kwenye kiti cha hukumu na kuleta ushahidi wa nchi nzuri. Nina furaha sana kwamba kulikuwako na watu miaka mingi iliyopita, waliopitia taratibu zote, wakapanda na kuimiliki hiyo nchi, na kupata ushahidi kisha wakarudi, kwamba kuna nchi ng'ambo ya mto. Amina. Nina furaha sana kwa jambo hilo.

72 Sasa, walifanya kosa lao baya sana walipoanza kumnung'unikia Musa, na kumnungunikia mtumishi wa Mungu, na kumnung'unikia Mungu, ndipo ikawapita. Basi kumbukeni, kila mmoja wao aliyenung'unika kamwe hakuingia kwenye nchi hiyo. Yesu alisema, wakati alipokuwa duniani, "Baba zenu walikula mana nyikani, lakini kila mmoja wao amekufa." Sawa. "Lakini Mimi ndimi Chakula cha Uzima kitokacho kwa Mungu Mbinguni ambacho mtu anaweza kukila na asife." Loo, napenda hilo. Kupita kutoka mautini kuingia Uzimani, kufanyika kiumbe kipya katika Kristo Yesu.

73 Mambo ya kimwili yalikuwa yamekatilia mbali ugavi wao wa kiroho, mambo ya kimwili yalikuwa yamekatilia mbali furaha yao yote, ninii yote. . . Ndipo wakaanza kunung'unika na kuzozana, wakawaingiza jangwani. Kama kuna kitu ninachochukia ni jangwa, kuna joto, hakuna mtu, ni vigumu, anayeweza kuishi huko, na kila kitu unachokikabili huko jangwani kina miiba juu yake, kila namna ya maskini mmea mdogo una miiba juu yake. Mnajua ni kwa nini? Ni kwa sababu hakuna maji huko. Sasa, kama mmea uo huo mdogo ulikua nchini mwangu, ama huko juu katika nchi iliyo na mvua, mmea huo mdogo usingekuwa ni mwiba. Maskini mwiba huo ungekunjuka, nao ungekuwa ni jani zuri, laini unapofikia mahali penye maji.

74 Hiyo ndiyo shida ya makanisa, kinachowafanya kuzozana, na kugombana, na kuleta fujo, na *wanajiita* Wakristo, kwa sababu wamepitwa kando na nchi ya baraka, wakatoka kwenye Chemchemi isiyokauka kamwe, wakatoka kwenye Mwamba katika nchi yenye uchovu. Nao wamekuwa wakavu na wa kimwili, wanataka kushikilia, na kusema, "Siku za miujiza zimepita. Hilo ni kundi la watakatifu wanaojibingirisha. Hakuna kitu kama hicho."

75 Loo, hebu waje tu kwenye maji wakati mmoja, wanakunjuka tu na wanakuwa wororo na watamu, na wema, na wanyenyekevu. Jambo fulani hutukia unapomtia majini, sijui ni kwa nini,

lakini linatukia hivyo. Loo, mambo ya kimwili yalikuwa yamewakatilia mbali.

76 Angalieni, hivi ndivyo walivyokuwa wamefanya: Walikuwa wameacha vyungu vya vitunguu saumu vya Misri wapate kula chakula cha Malaika, nao walikuwa wakilalamika. Ungeweza kuliwazia? Naam, tunaona jambo hilo. Walikuwa, pia, walikuwa wameyaacha maji ya Misri yenye matope wakaunywee Mwamba huo wa kiroho, wangali wakiulalamikia; walikuwa wamewaacha waganga wenye majivuno wa Misri, waliojivunia jinsi walivyokuwa wakuu, wapate kuwa pamoja na yule Tabibu mkuu, hata hakukuwako, hata nguo zao hazikuchakaa, wala hapakuwapo na mnyonge miongoni mwao walipotoka nyikani, wangali wakilalamika. Na halafu walikuwa wameondoka, pia walikuwa wamewaacha watu waliosema siku za miujiza zimepita, wapate kuwa pamoja na watu walio na ishara zinazowafuata, waaminio.

77 Sasa, si ni vivyo hivyo siku hizi? Mlitoka kwenye upuuzi huo wa kale, baridi wa kawaida, mkampokea Roho Mtakatifu, naye Mungu anawajaza na wema, nanyi mnainywea ile Chemchemi isiyokauka kamwe, na mambo hayo yote pale, furaha isiyosemeka na iliyojaa utukufu, na kisha mnaanza kulalamika; jambo lile lile tu. Muda si muda mwajua, mumepitwa jangwani. Hivyo ndivyo Mungu afanyavyo, ni hivyo tu. Ninii . . . Mungu hafanyi hivyo, watu hufanya hivyo wenyewe, mawazo yao wenyewe ya kimwili yanafanya hivyo.

78 Walikuwa wameona miujiza kumi yenye nguvu ikifanywa huko chini Misri: nzi, chawa, moto, malaika wa mauti, yote waliyokuwa wameona huko Misri, miujiza hii yote mikuu ambayo walikuwa wamemwona Mungu akifanya, na bado walikuwa ni watu wenye mawazo ya kimwili. Na ndipo wakaona Bahari ya Shamu iliyokuwa imesimama kwenye njia yao ya wajibu, walikuwa wakienda zao barabarani wakati huo, wakatoka, kulikuwa na Nguzo ya Moto mbele yao, nao wakasonga mbele hata kwenye Bahari ya Shamu, na walipofika huko, papo hapo kwenye wajibu wao palikuwapo na kizuizi. Basi muda si muda mwajua, hofu ikawashika, nao hawakujua la kufanya.

79 Hivyo ndivyo watu wafanyavyo siku hizi wakati hofu inapowashika wanapokuwa moja kwa moja kwenye wajibu wao. Sikiliza, ndugu, hebu niseme hivi: Kama unatembea katika Nuru, ukiwa na ushirika pamoja na Mungu, pamoja na watu Wake, na Roho Mtakatifu yuko juu yako, nawe unakutana na pingamizi papo hapo ukiwa kwenye wajibu, usisimame, endelea tu kukaza mwendo, Mungu atafanya njia kupitia kwake. Hilo ni moja ya matukio makuu sana ya maisha yangu, ni kumwona Mungu. Nisipoweza kupita juu yake, kuingia chini yake, kuizunguka, ama vyovyote vile, Mungu hufungua njia,

nami ninaipitia. *Kwa namna fulani* neema Yake inatosha kutupitisha humo.

80 Sasa, walifika hapo na kuona hiyo Bahari ya Shamu ikifunguka, nao...Lilikuwa ni jambo kubwa jinsi gani! Wangewezaje kunung'unika? Wangewezaje kulalamika baada ya kuona miujiza hiyo? Tunawezaje kulalamika leo baada ya kuona kile ambacho tumeona? Miamsho mikuu, kampeni za uponyaji, Roho wa Bwana akishuka, Mtambuzi.

81 Biblia ilisema Neno la Mungu...naye Yesu alikuwa ni Neno, "Hapo mwanzo alikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu." Mungu alijiweka Mwenyewe, ninii Yake Mwenyewe...kwa tabaka Lake, Mungu, aliyeumba dunia, akafanyika udongo, na kuishi duniani; Mungu, aliyefanya mwili, alifanyika mwili na kuishi katika mwili.

82 Loo, hilo linapaswa kuwavutia watu! Mungu angaliweza kutoka Mbinguni kwa gwaride kamili la Malaika kama angalitaka. Mungu angaliweza kushuka chini akiwa m—mtu mzima kabisa, Malaika wakiwa pande zote mbili, wakishuka kwenye ushoroba wa Mbinguni, wakipiga parapanda za Mbinguni, Yeye—Yeye angaliweza kufanya hivyo. Angeweza kuja akiwa mtu mzima, bali alichagua kuja Mtoto mchanga. Angaliweza kuzaliwa katika ikulu, angeweza kuumbwa Mbinguni kama angetaka, lakini alichagua kuja, bila hata kitanda cha kuzaliwa, alienda horini juu ya lundo la samadi, na juu ya lundo la samadi alichagua kuzaliwa.

83 Inapaswa kuvutia: Yehova akilia kama mtoto mchanga, Yehova akicheza kama mvulana, Yehova akifanya kazi kwa bidii kama mwanadamu. Loo, ni siri kuu! Ni ishara kuu kwa watu. Kila mtu akitaka ishara, hiyo ndiyo ishara kuu kuliko zote ambayo Mungu aliwahi kufanya, wakati Mungu alipofanyika mwili na kukaa miongoni mwa wanadamu, ishara kuu.

84 Hakika ingewavutia watu, bali wanakuwa wa kimwili, wanaondoka, "Loo, naam, nadhani hilo ni sawa." Loo, zaidi ya sawa, ni ukamilifu wa Mungu ukifanya kazi, akijifanya Mwenyewe, akivuka tabaka Lake, akitengeneza hema na kuishi katika hema Lake, akilitandaza miongoni mwetu, na kuishi jinsi tuishivyo. Amina. Hmm! Mungu! Hili hapa, bali halivutii usikivu, kanisa linakuwa la kimwili na kulikwepa, linalipitia juu, linayaacha mambo haya makuu.

85 Sasa, tunaona ya kwamba tayari walikuwa wameiona hii miujiza, angalieni kilichokuwa pamoja nao, walikuwa na Mwamba uliopigwa, wangeweza kuunywea, walikuwa na nyoka wa shaba kwa ajili ya uponyaji. Loo, jamani! Walikuwa na na—nabii aliyekuwa na Neno la Mungu, juu ya nabii huyo kulikuwako na Nguzo ya Moto iliyokuwa ikiongoza, wala hakuna hata wakati mmoja Hiyo iliwahi kuwapungukia.

86 Utukufu! Loo, na—najisikia kupaza sauti. Angalieni, haikuwa imeshindwa, Mungu hashindwi, Yeye hawezi kushindwa na abaki Mungu, Yeye angali ni Mungu. Mwamba uliopigwa, yule nyoka wa shaba, nabii, upatanisho, dhabihu, kila kitu neema ilikuwa imewaandalia tayari, na baada ya Mungu kufanya mambo hayo yote, walikuwa kama watu wengi sana siku hizi, hawana budi kubembelezwa kote. Mungu hataki watoto wachanga, Mungu anawataka wanaume na wanawake.

87 Ninaupenda ule ushuhuda wa mzee Buddy Robinson, yeye alisema, "Bwana, nipe uti wa mgongo ukubwa wa gogo la msumeno, uweke maarifa mengi kwenye ncha ya nafsi yangu, unijalie nipigane na ibilisi mradi tu nimesalia na jino moja, kisha nimwume kwa ufizi mpaka nife." Huo ndio tunaohitaji, ujasiri, si mfupa wa shingo ya kuku, bali uti wa mgongo, moyo halisi, uliojazwa na Roho, uliojazwa na Roho Mtakatifu, uliotakaswa kwa Damu ya Yesu Kristo, unaoishi katika maisha, ukitembea katika njia ya Mungu, ukizishika amri Zake, ukidai kila ahadi kama mali yako mwenyewe. Haleluya!

88 Loo, najua nina kichaa, lakini kama ungejisikia kama nilivyojisikia, ungetenda vivyo hivyo, vema, kwa sababu ni jema.

Mtu fulani alisema, "Jamani, umerukwa na akili!"

89 Vema, labda nimerukwa, lakini kama nimerukwa, niacheni tu. Nina furaha zaidi kwa njia hii kuliko nilivyokuwa vinginevyo, kwa hiyo hebu niache tu nibaki hivi.

90 Nilikuwa nikitembea mjini, nikamsikia mtu akisema wakati mmoja, kwamba mtu fulani alishuka kuja barabarani, alikuwa na maandishi mbele ya kifua chake, namna *hii*, kana kwamba alikuwa akishawishi, mahali fulani, alisema, "Mimi ni mpumbavu kwa ajili ya Kristo." Na mgongoni mwake, baada ya kupita, kaangalia nyuma, kasema, "Wewe ni mpumbavu wa nani?" Kwa hiyo nashangaa tu sasa!

91 Afadhali niwe mpumbavu kwa ajili ya Kristo, kumjua Yeye, nikijua jambo hili, ya kwamba ninamjua katika nguvu za kufufuka Kwake, kwamba siku moja wakati mauti yatakaponichukua, ule mkondo mkubwa wa mwisho ulioko kule, moyo wangu unadunda kila dakika, unaelekea kwenye mkondo huo, bali nitakapoufikia sitaki kuja kama mwoga, ninataka kutembea pale, na kujivika mavazi ya haki Yake, nikijua jambo hili, ya kwamba ninamjua katika nguvu za kufufuka Kwake, ya kwamba aitapo, nitatoka miongoni mwa wafu, nikiyaacha mambo hayo yaliyopita, nitakaza mwendo niifikie mede ya wito mkuu. Utukufu! Naam, bwana.

92 Ndugu, tunahitaji uamsho wa kale, wa Kipentekoste, wa misituni, unaoua dhambi uipige hii California, majimbo mengine yote, na mataifa, kote nchini, uzirudishe nguvu za Mungu kanisani tena. Tumefika Kadeshi, kiti cha hukumu, mambo haya yote, tungali tunazozana, tungali tunalalamika.

93 Nguzo ya Moto juu ya nabii, maneno yake yalikuwa makamilifu, Mwamba uliopigwa, nyoka ya shaba, miujiza na ishara, walizofanya kutoka kwake, halafu wangali wanalalamika. Loo, wakila tu chakula cha Malaika, na bado wangali kwenye kitunguu saumu, walitaka kurudi kwenye vile vyungu vya kale vya vitunguu saumu, ilionyesha hawakuwa tayari kuingia Kanaani, hiyo ni kweli.

94 Mwajua, mtu fulani alisema wakati mmoja...Nilikuwa nikihubiri, kulikuwa na mwanamke aliyekuwa akilia, naye alikuwa tu ameinua mikono yake na kulia, akimsifu Mungu. Roho Mtakatifu alikuwa pale, huyo mwanamke alikuwa amejazwa na Roho Mtakatifu. Sumaku inawezaje kuvuta chochote isipokuwa kimetiwa sumaku kwake? Hiyo ni kweli.

95 Kulikuwa na mtu aliyekuwa mfuasi wa kanisa lingine, rafiki yangu, alikuwa amesimama nje, akasema, "Billy, nilikuwa nikifurahia mahubiri yako mpaka yule mwanamke alipoinuka na kuanza kulia." Kasema, "Ungewezaje kamwe kuhubiri huku anafanya hivyo?"

Nikasema, "Huo ndio wakati pekee ninaoweza kuhubiri, ninapoona ya kwamba nguvu za Mungu zimelinyakua Kanisa, zikaunyakua ujumbe."

Akasema, "Ilifanya tu mitetemo ipitie mgongoni mwangu."

96 Nikasema, "Kama ungepata bahati ya kutosha kuingia Mbinguni, ungeganda hata kufa, kwa sababu wanalia, na kupiga makelele, na kumsifu Mungu, mchana na usiku. Malaika wakiruka huku na huko, wakilia, 'Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu, kwa Bwana! Mtakatifu...' Sasa, hebu nikwambie jambo fulani sasa hivi, ndugu yangu, unaishi katika ulimwengu mnyamavu sana utakaowahi kuishi." Amina. "Ukienda kuzimu, kutakuwa na kulia, kuomboleza, na kusaga meno. Ukienda Mbinguni, kutakuwako na haleluya na sifa za Mungu, mchana na usiku, wakati wote na Umilele wote. Hapa ndipo mahali panyamavu sana ulipowahi kuishi." Naam.

97 Loo, jinsi Mungu anavyotaka kulibariki Kanisa Lake! Wameona mambo hayo yote na bado wana nia ya kimwili. Jinsi walivyosahau miujiza hiyo yote upesi wakati ja—jambo jipya lilipoibuka! Wakati jaribio jipya lilipokuja, walisahau yote waliyokuwa wameona.

98 Tunafanya hivyo, tukiwa na mkutano, nguvu za Mungu zitashuka, ishara kuu na maajabu yatatukia, ndipo Shetani anaweza kuja na kubandika kitu juu yako, usahau ya kwamba huyo ni Mungu wa Mbinguni aliyekuwa tu akikufanya upaze sauti, akikufanya umsifu Bwana, unamsahau Mungu wa Mbinguni aliyekutoa katika...kama kinga cha moto, unamsahau Mungu wa Mbinguni aliyekuchimbua kutoka mashimoni, kutoka kwenye mwamba ulikochimbuliwa, ni rahisi kumsahau.

99 Hebu nikwambie, ndugu yangu, tunachohitaji usiku wa leo ni mtu mwenye dhamira ya chuma, atakayesimama pale katika nguvu za Roho Mtakatifu, haidhuru ni nini kijacho ama kiendacho, angali anaipeperusha ile bendera ya ushindi akielekea kwenye Nchi ya Ahadi. Tunahitaji, usiku wa leo, kanisa la namna hiyo, Kanisa hilo lisiloghoshiwa, lililotakaswa kwa Damu ya Yesu Kristo, lililotiwa mafuta kwa Roho Mtakatifu, kwa ishara na maajabu, ukelele wa—wa Mfalme kambini wakienda zao, wakisonga mbele, naam, bwana.

100 Haya yote, licha ya mambo haya yote ya kimwili waliyokuwa wamefanya, kote jangwani mahali pale, kama vile makanisa mengi yalivyo usiku wa leo, Wapentekoste wengi kule, wakati mizigo mizito ilipokuja na watu wakaanza kulia, "Loo, ingekuwa heri kwa Mungu kama tungalifia huko Misri," sasa nini kilitokea?

101 Mungu alimwita Musa na Haruni katika, Mbele Zake, akashuka katika Utukufu wa Shekina na kuwabariki, Mungu akamwambia nabii, kasema, "Nenda, ukanene na Mwamba," amina, katikati ya dhambi zao zote.

102 Kama Mungu alitaka kuweka hukumu juu yetu, hakuna mmoja wetu, ila ambaye amelalamika, tunastahili kwenda jehanamu, hatustahili uponyaji wetu, hatustahili wokovu wetu. Lakini katikati ya hayo yote, Mungu yeye yule aliyewasamehe dhambi zao na mashaka yao yote, Yeye angali alisema, "Sema na Mwamba, nao utatoa maji Yake." Amina. Hiyo ni kweli. Haidhuru ni jambo gani lililotukia, bado sema na Mwamba, katika dhambi zao, bado sema na Mwamba.

103 Moja kwa moja katika siku ambayo makanisa yote yanazozana na kugombana sana, moja linalosema, "Mimi ni *hiki*," na hilo lingine, "Mimi ni *kile*," na moja ni *hiki*, *kile*, na *kinginecho*, "Usiwe na uhusiano wowote *nao* na *kile*," Mungu yuko moja kwa moja katikati ya hayo yote, angali anamtuma Roho Wake Mtakatifu, angali anatuma nguvu Zake, angali anawaponya wagonjwa, angali anaonyesha ishara ya Masihi akiishi miongoni mwa watu, yeye yule jana, leo, na hata milele, katikati ya ugomvi wetu wa kimwili, na kadhalika.

104 Waangalie, wengi wao walisema, "Vema sasa, kama hayo ndiyo yote unayoweza kufanya! Sisi hapa tumepiga kambi jangwani, tumechimba katika kila chemchemi, tumechimba kwenye kila oasisi, wala hakuna maji."

105 Na hata hivyo mahali pakavu sana katika jangwa lote palikuwa ni ule Mwamba wa kale uliokuwa pale juu ya kilima, "Nenda ukanene na Mwamba." Jinsi Mungu anavyofanya mambo! Linatatanisha tu watu wa kimwili, hawajui tu la kufanya kulihusu.

106 Sasa, mahali pakavu sana jangwani ni mwamba, mtu yeyote anajua hilo. Vema, kama hakuna . . . kama hawawezi kupata maji

yoyote katika chemchemi za kale, basi watayapataje kwenye mwamba?

107 Kama hawawezi kupata uponyaji wa Kiungu katika lile kanisa *kuu* lenye jina *hili*. . . "Kama kuna uponyaji wowote wa Kiungu ungekuwa katika kanisa hili *kuu* tunaloshiriki, ama ungekuwa katika kanisa hili *kuu* tunaloshiriki, ile chemchemi ya kale, utawezaje kamwe kupata moja sasa, kupanda juu ya mlima na kuzungumza na mwamba huo wakati kwanza kabisa hamna maji huko juu?" Lakini jambo ni kwamba, si jinsi unavyoonekana, ni kumwamini Mungu kwa Neno Lake, kusema, kwa vyovyote vile.

108 Kama daktari akikukataa, kasema, "Kansa hiyo itakuua, ingekuwaje ninii yoyote. . . mtu kukuwekea mikono?"

109 Haileti tofauti yoyote jinsi inavyoonekana, jinsi inavyoonekana ya kipumbavu kwa sayansi, Mungu alisema, "Wataweka mikono juu ya wagonjwa, nao watapata afya," haidhuru inaonekanaje.

110 "Unamaanisha katika siku kama hii ambapo tuna utamaduni wote, na ninii yote—ninii yote, utamaduni huu. . . " Daima niliwazia juu ya utamaduni, naam, hilo—hilo ni jambo kuu, uh-huh, vema, maoni ya—yangu kuhusu utamaduni ni mtu ambaye hana ujasiri wa kutosha kumwua sungura, lakini anaweza kumla akalijaza tumbo baada ya mtu mwingine kumwua. Sasa, hiyo ni. . . Loo, jamani! Tunachohitaji siku hizi si utamaduni, tunachohitaji leo ni Roho Mtakatifu kuleta imani ndani yetu kwa Neno la Mungu aliye hai. Hiyo ni kweli kabisa.

111 Katika siku hii kuu ya elimu, siku hii kuu ya sayansi, hiyo ina maana gani kwa Mungu? Mbona, wao. . . Sayansi, wakati mmoja, ilijenga m—mnara mkubwa mno, ulikuwa ufike mpaka Mbinguni, naye Mungu akaketi tu na kuucheka ujinga wao. Basi jambo alilofanya, Yeye alituma mwenendo mdogo wa lugha kule chini na kukitatanisha kitu hicho chote. Loo, Mungu anaweza tu kufanya atakalo, sivyo? Loo, Yeye ni Mungu, Yeye ni Mungu milele, bila shaka.

112 Angalia kilichotukia hapa, sasa, tunapoona ya kwamba Mungu alimwambia Haruni katikati ya hayo yote, yeye na Musa, "Nenda, ukaseme na Mwamba, nao utatoa maji Yake."

113 Ni upumbavu jinsi gani, hiyo nia ya kimwili, "Vema, kama hicho ndicho bora sana unachoweza kunipa, achana nacho."

114 Kama vile Eliya, siku moja wakati alipoenda kuomba, naye akamtuma mtumishi wake aende aone kama kulikuwa na dalili yoyote ya wingu. Alienda mara ya saba, aliporudi alisema, "Loo, naam, kuna wingu dogo, karibu ukubwa wa mkono wa mtu, huko magharibi kule."

115 Akasema, "Simamisheni pipa la mvua, nasikia sauti ya mvua nyingi ikija." Ilikuwa ni kitu gani?

116 Mbona, ninii—mbona, nia ya kimwili ingelishika hilo upesi, na kusema, "Vema, kama hilo ndilo bora uwezalo kunipa! Kama hayo ndiyo yote unayoweza kufanya!"

117 Loo, ndugu, ni ishara zaidi jinsi gani tuliyo nayo ya Mungu aliye hai miongoni mwetu usiku wa leo! Jinsi ambavyo tume—tumepita kutoka mautini kuingia Uzimani, ubatizo wa Roho Mtakatifu umekuja juu yetu, Yesu anatuponya, Yesu anatuokoa, Yesu anajaza na Roho Mtakatifu, Yesu hushuka na kuonyesha miujiza, anaupambanua moyo, anafanya ishara, ile Nguzo ya Moto, picha zilizopigwa, Yuko hapa sasa, Yesu yule yule aliyekuwa jana, ni yeye yule jana, leo, na hata milele!

118 Yesu alisema, alipoulizwa, alisema, "Wewe ni mtu hujapata bado miaka hamsini, nawe unasema umemwona Ibrahimu?"

119 Akasema, "Ibrahimu asijakuwako, MIMI NIKO." Na MIMI NIKO alikuwa ile Nguzo ya Moto iliyomwongoza Musa kupitia nyikani.

120 Wakati alipokuwa duniani, Yeye alisema, "Nilitoka kwa Mungu na ninaenda kwa Mungu. Bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona tena, bali ninyi mtaniona kwa kuwa Mimi," *Mimi* ni kiwakilishi nafsi, "nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari." Sawa.

121 Na wakati alipokufa, akazikwa, akafufuka, yapata majuma machache baadaye, Sauli alikuwa akienda zake Dameski, ndipo Nguzo kuu ya Moto, iliyowaongoza wana wa Israeli, ikashuka mbele zake pale, ikayapofusha macho yake, Akasema, "Sauli, Sauli, mbona unaniudhi?"

Kasema, "U nani Wewe, Bwana?"

122 Akasema, "Mimi ni Yesu, na ni vigumu kwako kuupiga teke michokoo." Ilikuwa ni kitu gani? Alitoka kwa Mungu, akaishi katika mwili, akarudi kwa Mungu. Nguzo ile ile ya Moto, Roho Mtakatifu yeye yule yuko pamoja nasi usiku wa leo, akifanya kazi zile zile, ishara zile zile, kila kitu kingine kile kile, akithibitisha ya kwamba ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Huyo mwanamke angeweza kugusa upindo wa vazi Lake, loo, mtu anaweza kuambiwa yeye ni nani, amefanya nini, jinsi ya kuliondokea, yote kwa nguvu za Mungu aliye hai anayeishi miongoni mwa watu Wake. Amina. Vema.

123 Hata hivyo, "Sema na Mwamba." Hebu na tuangalie baadhi ya watu walionena na Mwamba. Hebu tuone kilichotukia. Mtu wa kwanza aliyepata kunena na Mwamba alikuwa ni mtu aliyefungiwa katika theolojia fulani, alijitengenezea seti ya majani ya mtini, Adamu, akawazia, "Hayo yatafanya kazi tu kama chochote kile." Lakini alipokutana uso kwa uso na Mungu, aliona kwamba alikuwa uchi. Alifanya nini? Alinena na Mwamba, nao Mwamba ukamfanyia mlango wa kutokea, ule Mwamba uliokuwa katika Edeni.

124 Kulikuwako na Nuhu, mtu mwingine aliyekuwa amehubiri, nao watu wakampuuza na kumcheka, siku moja alinena na Mwamba, ndipo Mwamba ukamwingiza ndani ya safina, ukamweka mikononi Mwake, na kumpandisha juu ya dhoruba, na kuuzamisha ulimwengu wa mateso. Naam, bwana, Nuhu.

125 Kulikuwa na mtu jina lake Danieli wakati mmoja, aliyekuwa katika tundu la simba. Alishuka akaenda Babeli, naye akasema nafsini mwake kwamba hatajitia unajisi kwa chakula cha mfalme, hatakuwa na uhusiano wowote na ulimwengu, ingawa ilimbidi kuishi miongoni mwa watu hao, lakini hatajitia unajisi, alikusudia moyoni mwake hatajichafua. Basi siku moja mfalme akamtupa katika tundu la simba kwa sababu alikuwa akitekeleza wajibu wake, bali akanena na Mwamba, ndipo hiyo Nguzo ya Moto ikashuka na kuwazuia simba wasimkaribie usiku kucha kwa sababu alinena na Mwamba kabla hajaingia shimoni.

126 Kulikuwako na wale wana wa Kiebrania ambao hawangezisujudia sanamu za Mfalme Nebkadreza, nao wakawatupa katika tanuru ya moto, nao wakanena na Mwamba, naye yule Mtu wa nne alikuwa amesimama katika tanuru ya moto mle, Mwamba wa Miaka. Haleluya! Daudi alisema, "Kama nikifanya kuzimu kitanda, Yeye atakuwa huko. Nikizitwaa mbawa za asubuhi, na kuruka niende . . . "

127 Mwangalie Hajiri, alikuwa amefukuzwa nyumbani kwake, alikuwa na maskini mvulana mdogo anayenyonya, Ishmaeli, alitoka akaenda jangwani, hana mahali pa kwenda, maji yalikuwa yamekwisha, angefanya nini? Alikuwa amelelewa katika nyumba iliyoifahamu ule Mwamba, naye alifanya nini? Hakutaka kumwona huyo mtoto akifa, kwa hiyo akamchukua maskini jamaa huyo mdogo, akamlaza chini ya mti, kisha akaenda umbali wa kurusha mshale kutoka kwenye uta, akapiga magoti, naye akanena na Mwamba, nao Mwamba ukatoa maji Yake, basi mtoto huyo akaokolewa.

128 Na hata leo hii, Beerlahairoi ingali inasimama pale, chemchemi ile, ambayo ni "Mungu Ambaye ameniona." Alinena na Mwamba kwa ajili ya mtoto wake anayekufa.

129 Je, unaweza kuzungumza na Mwamba usiku wa leo? Je, uko tayari kuzungumza Naye? Je, unajua lolote kumhusu?

130 Yoshua, alitembea tu, akavuka Yordani baada ya kufanya uamuzi huo mkuu, akawatuliza watu, akasema, "Tunaweza kuiteka."

131 Mungu akasema, "Yoshua, wewe ndiwe unayejua yote kuihusu, nitakuacha tu uwaongoze watoto tangu sasa na kuendelea."

132 Akaenda kwenye kampeni yake ya kwanza, akaufikia ukuta wa Yeriko, akauzunguka, na kusema, "Sasa, nitaupandaje? Nitazipandaje hizo kuta? Zina mawe hayo yote, na kadhalika, yamewekwa huko juu, nyuta zao, na kadhalika, tayari kurushwa,

nasi hapa nje hapa, sana sana hatuna silaha, ni zile tu tulizookota kutoka kwenye nyara kote katika safari yetu, na sisi hapo. Nitafanyaje jambo hilo?" Ndipo baada ya kitambo kidogo akamwona Mtu amesimama amechomoa upanga Wake. Akasema, "U nani Wewe? Je, Wewe ni adui yetu? Wewe ni mmoja wetu?"

133 Akasema, "La, mimi ni Amiri wa jeshi la Bwana."

134 Basi Yoshua akanena na Mwamba. Ndipo ukelele ukapigwa, nazo hizo kuta zikaanguka, maana alinena na Mwamba.

135 Miaka mia kadhaa baadaye tangu wakati huo, kulikuwa na maskini ombaomba kipofu ameketi juu ya baadhi ya mawe hayo yaliyokuwa yameporomoshwa kutoka kwenye ukuta huo. Loo, jamani, kule kunena kwa Mwamba kulikuwa kumeelezewa vibaya kukaondoshwa kanisani, "Hapakuwepo na kitu kama hicho." Lakini alikuwa ameketi pale kipofu, akiwazia juu ya barabara hiyo, wakati alijua ya kwamba Elisha na Eliya walipitia barabara iyo hiyo, wameshikana mikono, wakienda Yordani. Mbele tu ya hapo Yoshua alikuwa ameongea na huyu Amiri wa jeshi la Bwana. Akasema, "Loo, kama ningaliishi katika siku hiyo ningalisema Naye, pia." Na yapata wakati huo kelele zikaanza kutokea.

136 Mwajua, kwa kawaida mahali Mungu alipo pana kelele nyingi sana, sijui ni kwa nini, lakini kuna kelele nyingi sana popote Mungu anapokuja. Huyu hapa Amiri yuyo huyo wa jeshi la Bwana anakuja. Watu walijaribu kumfanya anyamaze, lakini alinena na Mwamba, nao Mwamba ukamrejeshea macho yake. Yeye . . .

137 Walijaribu kumfanya anyamaze, wakajaribu kumnyamazisha. Ameketi pale akitetemeka, maskini miguu yake mitupu, imewekwa pale kwenye jua hilo na maskini mikono yake iliyoparara na—na koti lake kuukuu, lililochakaa, lakini akajirushia koti hilo kutoka upande mmoja hadi mwingine, kisha akaondoka. Kwa nini? Alikuwa tayari kusema na Mwamba, nao Mwamba ukamrejeshea macho yake. Haleluya!

138 Hilo ni onyo kwa kila kipofu humu ndani usiku wa leo, kama wewe ni kipofu kiroho, au kipofu kimwili: Nena na Mwamba. Yeye ni Mwamba unaorejesha macho. Amina. Semeni na Mwamba. Naam, bwana. Yule kipofu . . .

139 Kulikuwa na mwanamke wakati mmoja, aliyetoka akaenda kisimani kuchota maji, alikuwa katika hali mbaya, alikuwa kahaba, akamwona Mtu ameketi pale ameegemea ukutani, wala hakujua Yeye alikuwa ni Nani.

140 Baada ya kitambo kidogo akasema, "Mwanamke, nipe maji ninywe." Akaanza kuzungumza naye, mpaka akapata kujua shida yake ilikuwa ni nini, akasema, "Nenda, kamwite mumeo."

Akasema, "Sina."

"Mbona," Yeye akasema, "hiyo ni kweli, umekuwa na watano, na yule unayeishi naye sasa siye mume wako."

Akasema, "Bwana, naona ya kuwa Wewe ni Nabii. Tunajua ya kwamba kuna Mwamba unaokuja siku moja, unaoitwa Masihi, Naye atafanya jambo hili."

Akasema, "Mimi ninayesema nawe Ndiye."

141 Ninaweza kumwona akiangusha mtungi huo wa maji, macho yake makubwa, mazuri yakiangaza, akaingia mjini akijua ya kwamba alikuwa amesema na Mwamba. Haleluya! Naye akapata Maji asiyokuja kwenye kisima hicho kuchota. Loo, alikuwa amesema na Mwamba.

142 Maskini Martha, wakati mmoja ndugu yake alikuwa amekufa, naye akazikwa, siku nne huko nje kaburini, tayari anaoza, mabuu ya ngozi yakila mwilini mwake, naye akasikia kulikuwa na kitu fulani mjini, kwamba Yesu alikuwa amekuja. Akatoka akaenda kule alikokuwa, akaanguka mbele Zake, naye akasema, "Bwana, kama ungalikuwa hapa, ndugu yangu asingalikufa, lakini hata sasa, Bwana, lolote utakalomwomba Mungu, Mungu atakupa."

Akasema, "Ndugu yako atafufuka tena."

143 Kwa nini? Alinena na Mwamba, amina, nao ukaleta mauti kutoka kwenye uharibifu, na kukemea mauti na kuleta uzima. Ambapo mtu aliyekuwa amekufa siku nne, akasimama kwa miguu yake, na akaishi tena, kwa sababu alisema na Mwamba.

144 Wanafunzi usiku mmoja walikuwa huko nje baharini, matumaini yote yalikuwa yamekwisha, na nini kilitukia? Waliona Kitu fulani, kilionekana kama kivuli kikiwajia, nao wakaona kwamba ilikuwa ni ule Mwamba, nao wakanena na Mwamba, matumaini mapya yakaingia, nao hao wakaondoka, na kitu hicho chote kiliokolewa kwa sababu walinena na Mwamba.

145 Yairo, maskini yule kuhani, binti yake alikuwa amekufa, matumaini yote yalikuwa yamekwisha, papo hapo ikatokea aliwazia jambo fulani. Mke wake akamwona akikimbia, akaitwaa kofia yake, "Kwani unaenda wapi, Yairo?" Daktari alikuwa akiondoka nyumbani, amemtangaza amekufa, moyo wake umesimama, hana kupumua tena, amekuwa mgonjwa kwa siku kadhaa, sasa ameaga dunia. Akasema, "Kwani unaenda wapi sasa? Kwa nini ukaitwaa kofia yako?"

146 "Ilitokea tu kwamba nimewazia, nitaenda kuzungumza na Mwamba." Ndipo Mwamba ukaurejesha uhai tena ndani ya binti yake. Haleluya! Huyo ndiye Mungu wetu.

147 Kama unahitaji uhai, sema na Mwamba; kama unahitaji furaha, sema na Mwamba; kama unahitaji uponyaji, sema na Mwamba; kama unahitaji Roho Mtakatifu, sema na Mwamba; chochote unachohitaji, sema na Mwamba, Naye atatoa maji Yake. Mnaamini hilo?

148 Kile kanisa linachohitaji usiku wa leo, ni kurudi katika hali ya kuweza kusema na Mwamba, ule Mwamba wa Miaka, Kristo Yesu, Mwamba wa Mungu uliopigwa, Huo ni Mwamba wa Mungu, ni wokovu wa Mungu. Hiyo ingali ndiyo amri yetu usiku wa leo, ni chochote tunachohitaji, tuseme na Mwamba, na kutumia Jina la Mwamba, ndipo Mungu atatoa maji Yake kutoka kwenye Mwamba huo. Whiu! Utukufu!

149 Najisikia kama ningeweza kukimbia maili mia moja. Kwa nini? Loo, ndugu, ninajua ule Mwamba uliopigwa umewekwa papa hapa sasa. Usiupige tena, sema tu nao, sema tu na Mwamba, nao utatoa maji Yake. Mnaamini hilo?

150 Na tuinamishe vichwa vyetu na kuzungumza Naye basi. Chochote unachohitaji, sema na Mwamba huo, uone kama Yeye atatoa maji Yake.

151 Ee Mungu, uturehemu, tunajua ya kwamba Wewe ndiwe Mwamba katika nchi yenye uchovu, Wewe ni Kimbilio wakati wa dhoruba. Si ajabu Yesu alisema, "Wakinyamaza, mwamba huu utapiga kelele mara moja." Miamba!

152 Yohana alisema, "Mungu anaweza katika mawe haya kumwinulia Ibrahimu watoto." Mungu, jinsi tunavyokushukuru ya kwamba tunaweza kusema Nawe, tunashukuru sana kuwa tuko katika hali ya kuweza kuzungumzana. Damu ya Yesu Kristo inatuweka katika hali hii. Ninaomba, Baba, ya kwamba Wewe usamehe kila dhambi ya watu humu ndani. Tuchukue sote pamoja usiku wa leo, Baba. Tusamehe dhambi zetu, ponya magonjwa yetu. Bwana Mungu wa Mbinguni na aonyeshe nguvu Zake na utukufu Wake juu ya watu hawa.

153 Huku tumeinamisha vichwa vyetu, sijui kama kuna mmoja humu ndani asiyemjua Yeye, na angetaka kusema Naye kwa, kama Mwokozi wako. Waweza kuinua mkono wako? Useme, "Bwana Mungu, unirehemu na unipe Uzima wa Milele. Mimi. . . " Mtainua mikono yenu? Mungu akubariki, bwana. Kunaweza kuwa na mwingine? Mungu akubariki, mama. Kungekuwa na mwingine? Mtu mwingine? Mungu akubariki huko nyuma, dada. Mwingine aseme, "Ningetaka kusema na Mwamba, Ndugu Branham. Je, unamjua?"

154 Naam, ninamjua Yeye. Ninafahamiana Naye, Yeye ni Rafiki yangu, Yeye ni Mwokozi wangu. Nilisema Naye miaka thelathini na mmoja iliyopita, amesamehe dhambi zangu zote, ameponya magonjwa yangu yote, Yeye hunipa amani na utoshelevu.

155 Je, ungetaka nizungumze Naye kwa ajili yako, kwamba ungetaka kumjua Yeye, pia? Mtu mwingine inua mkono wako, useme, "Mimi, Ndugu Branham, ningetaka kumjua Yeye." Inua tu mkono wako, useme, "Niombee, Ndugu Branham." Hakika nitafanya hivyo. Bwana awabariki.

156 Je, kunaweza kuwa na mwingine kabla hatujafunga? Mungu akubariki huko nyuma, bwana. Hilo ni zuri, huko ni

kushawishika halisi. Mungu akubariki hapa, bwana, mkono wangu wa kushoto. Mungu akubariki, huo jamaa mdogo huko nyuma, mvulana mdogo, Mungu awe pamoja nawe, mwanangu, akufanye mhubiri. Mtu mwingine aseme, "Ningetaka kusema na Mwamba"? Vema. Hakuna mwingine? Mungu akubariki huko nyuma, niliuona mkono wako wakati uo huo. Ninangojea tu kwa dakika moja kuona kama kuna mtu mwingine.

157 Wazia hilo sasa. Uko jangwani? Hivi hujui pa kwenda? Je, umekuwa . . . umeondoka kwenye njia halisi inayopitiwa? Mbona usiseme na Mwamba? Atatoa maji Yake. Mwamba huo uliopigwa ulikuwa ni Fimbo ya hukumu ya Musa, fimbo ya hukumu ya Mungu iliupiga Mwamba huo, nao ukawa na ufa ndani Yake. Na kutoka kwenye Mwamba uo huo wakapata asali siku moja. Loo, jamani!

158 Hukumu ya Mungu ilimpiga Yesu Kristo, aliyekuwa Mwamba wa wokovu wetu, kuna ufa ubavuni Mwake, asali iko kwenye Mwamba, kama tulivyosema asubuhi ya leo. Wanapata chakula, unapata mahali pa kujificha wakati wa dhoruba, unapata uponyaji kwa ajili ya mwili wako. Unaona (Mungu ambariki msichana huyu mdogo aliyeketi hapa.), tafuta chochote unachohitaji, kiko kwenye Mwamba.

159 Kama tu utamwamini sasa kwa moyo wako wote! Vema. Niliuona mkono wako kule nyuma, tena. Ninangojea tu, ninangojea kuona kile Roho Mtakatifu atasema. Vema. "Kama unaweza kuamini!" Vema.

160 Baba yetu wa Mbinguni, Wewe unaona mikono yao, wanataka kusema Nawe. Ninawaleta katika Uwepo Wako, Bwana, jalia huu uwe ndio ule usiku, Mungu, kesho huenda ikawa imechelewa sana. Hapo . . . Huenda tusiwe, hakuna mmoja wetu atakayekuwa hapa kesho. Tunajuaje ya kwamba jambo hilo kuu haliendelei sasa kuanzisha kulipuliwa kwa ulimwengu? Tunajuaje ya kwamba kombora halitaachiliwa mahali fulani, nalo litasababisha kurushiana makombora? Wakati huo utakapoanza, Kanisa litakuwa likielekea Utukufuni, Ee Mungu, litanyakuliwa na kuvuka Yordani, Yordani ya mauti, nalo litaingia Utukufuni.

161 Jalia Uwepo Wako ujulikane kwa watu hawa usiku wa leo, Baba. Jalia wajue ya kwamba Huyu ambaye wamemwinulia mikono yao, angali ni Bwana Mungu yeye yule, Yeye habadiliki, watu hubadilika, nyakati hubadilika, bali Mungu habadiliki. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

162 . . . njoo huku juu. Na mmoja wa wahudumu hapa, hao ndugu . . . Wakati mwingine katika ibada hizi za uponyaji, ninakuwa dhaifu sana hata siwezi kuona mahali ninaposimama, na mwanangu, ama Leo, ama Gene, ama baadhi yao watakuja, waniguse ubavuni na kunitoa nje. Ni kwa sababu maono hayo yananidhoofisha sana, ni vigumu kwangu kusimama

hapa. Unaona? Hiyo ndiyo sababu nafikiri inatosha na zaidi. Nami ninakutumaini wewe, ndugu, wewe dada, wewe ambaye umeinua mkono wako, wewe usiyemjua Mungu, ni wokovu wako. Mungu tayari ameniokoa, bali nisingeweza kuridhika isipokuwa umeokoka, nataka uende, pia, nataka uwe Huko.

163 Sasa, Mungu haninii—Mungu hafanyi mambo ili tu . . . Kama ningeweza kusimama usiku wa leo, na kusema, “Nitawaambia ni nani atakayekuwa rais,” na kuwaambia hasa, na iwe hivyo, vema, baada ya kitambo kidogo mngesema, “Ndugu Branham ni nabii mkuu. Hakika, alisema ni nani hasa angekuwa rais.” Lakini mnajua nini? Ingefaa nini? Mnaona? Lisingemtukuza Mungu hata kidogo, hilo lingenitukuza mimi. Mnaona? Kwa hiyo, Mungu hafanyi mambo hayo namna hiyo, Mungu hafanyi hivyo, Yeye hufanya tu mambo kwa ajili ya utukufu Wake.

164 Yeye—Yeye humruhusu nabii kuingia mahali ambapo hata nabii wakati mwingine hufikiri ni yeye mwenyewe. Kama vile Daudi katika Zaburi ya 22 alivyolia, “Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha?” Maneno yale yale aliyosema Yesu msalabani. Ilikuwa ni kitu gani? Roho wa Kristo ndani yake alimtia mafuta, naye akanena Maneno ya Kristo.

165 Mwangalieni I—Isaya, jinsi alivyonena na kuwazia ya kwamba ilikuwa ni yeye, Masihi alikuwa ndani yake *sana*. Mwangalie Daudi akipanda juu ya mlima, akiangalia nyuma juu ya Yerusalemu, akilia kama mfalme aliyekataliwa, miaka mia chache tu baada ya hapo, Mwana wa Daudi alipanda juu akiwa Mfalme aliyekataliwa, akiangalia nyuma juu ya Yerusalemu akilia, “Yerusalemu, Yerusalemu, ni mara ngapi nimetaka kuwakusanya pamoja, kama vile kuku awakusanyavyo vifaranga vyake, lakini hamkutaka!” Wazia hilo. Sasa, huyo ni Roho wa Mungu. Sasa, Mungu huwatumia manabii Wake kumtukuza Yeye. Mnaamini hilo?

166 Sasa, mstarini hapa usiku wa leo, sidai kuwa mponyaji yeyote, mimi si mponyaji, Mungu ndiye Mponyaji. Yote ambayo Mungu anaweza kukufanyia, tayari ameyafanya, sasa jambo la pili unalopaswa kufanya ni kuwa na imani ya kukubali yale Yeye amefanya. Yeye amekupa ahadi, anataka uingie. Sasa, ni wangapi wanaoamini ya kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele? Asanteni. Ni wangapi wanaojua ya kwamba Yeye ni Kuhani Mkuu, sasa hivi, anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu?

167 Ungejuaje ulimgusa, kama ulimgusa? Vema, Yeye . . . Huyo Kuhani Mkuu angetendaje? Kama vile alivyofanya jana. Hiyo ni kweli? Angekuwa vivyo hivyo. Kama ungeweza kumgusa kutoka mahali ulipo sasa hivi, na kugusa upindo wa vazi Lake, basi kama Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele, angegeuka moja kwa moja pamoja na Roho Wake na kufanya jambo lile lile alilomfanyia yule mwanamke aliyemgusa. Hiyo ni

kweli? Akaangalia nje mpaka akaona kwamba alikuwa ni nani, kulikuwako na umati mkubwa wa watu pale wakimgusa, bali Yeye aliangalia kwenye kusanyiko hilo mpaka akaona kwamba alikuwa ni nani, akasema, "Imani yako imekuokoa. Kutokwa kwako na damu kumekwisha." Mnaona? Alijua jambo hilo.

168 Sasa, ni kitu gani kilichosababisha hilo? Alimgusa Kuhani Mkuu. Unaweza kufanya jambo lile lile usiku wa leo, kama Yeye ni Kuhani Mkuu yeye yule. Kama ni Nguzo ile ile ya Moto, kama picha hii tuliyo nayo hapa, wakati mwingine ninaziweka hapa, bali picha ya Malaika wa Bwana, kama Huyo ni Malaika yule yule wa Bwana, Yeye atafanya jambo lile lile. Kama ni yeye yule jana, leo, na hata milele, itazaa Uzima Wake.

169 Aisee, ni wangapi wanaouhisi Uwepo wa Mungu? Unanirarua tu vipande-vipande hapa kwenye jukwaa hili. Hiyo ni kweli, marafiki. Hata sininii. . . Ninaamini hata haitubidi kuwa na mstari wa maombi. Ni wangapi wanaoamini ya kwamba Mungu anaweza kukuita moja kwa moja kutoka nje, hata uwe nani, na kukuponya sasa bila mstari wa maombi? Kama utaamini kwa moyo wako wote, Mungu atafanya hivyo. Vema. Utaamini kama atafanya hivyo? Utamwamini, umkubali? Vema.

170 Ni wangapi walio wagonjwa hapa ndani? Inueni mikono yenu. Ni wangapi wanaomtaka Mungu maishani mwako kwa ajili ya uponyaji? Inueni mikono yenu. Sasa, wangapi wenu ni wageni kwangu? Inueni mikono yenu, kwamba sijui lolote kuwahusu, inueni mikono yenu. Vema. Sasa ninyi ombeni. Msininii. . . Wewe mwombe Kuhani Mkuu na kugusa vazi Lake, uone kitakachotukia.

171 Loo, kama Yeye atafanya hivi! Sijui atafanya hivyo, ni—ninatumaini ya kwamba atafanya hivyo. Ninaamini ule upako, Nguzo ile ile ya Moto iko hapa usiku wa leo, ninaamini hilo. Ninaamini kwa moyo wangu wote. Yeye alisema, aliniambia, aliniambia ya kwamba ita—itatendeka. Ninamwamini kwa moyo wangu wote, ninamwamini.

172 Shetani, afadhali uondoke kwa sababu sisikilizi yoyote ya takataka zako. Ninaamini Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele, Biblia Yake iliahidi hilo, na Yeye ni yule yule, watu wanaweza kumgusa.

173 Bwana Mungu, jalia lithibitishwe usiku wa leo. Jalia Roho Mtakatifu alithibitishe, ya kwamba Wewe ni Bwana Yesu yeye yule, ya kwamba unaweza kuguswa. Tujalie, Bwana. Mtumie mtumishi Wako mnyenyekevu, Bwana Mungu, nena na hawa watu kupitia kwangu, kama unaweza kutumia sauti yangu, mimi hapa, Bwana. Kama unaweza kutumia imani yao, nena, Bwana, ipate kuwatia wengine moyo. Jalia mtu akuguse Wewe, Bwana, ili kwamba wajue ya kwamba Wewe ni Mwamba ule ule wa Miaka, Wewe ni Mwamba ule ule utakaotoa maji Yake mara

tu usemapo Nao. Kwa kuwa ni Kuhani Mkuu sasa anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu. Tujalie, Bwana. Na iwe hivyo, katika Jina la Yesu.

174 Amini tu, ingia tu kwa uchaji, na uamini. Sasa, siwezi kufanya hivyo, imani ye—yenu ndiyo haina budi kufanya hivyo. Iweni tu na imani, kwa unyenyekevu. Msisukumane, msisukumane, tulieni tu, useme, "Naam, Bwana, ninakuamini Wewe, ninakuja Kwako, Bwana. Mtu huyo hanijui. Angenijuaje? Yeye ni mgeni kwangu. Sasa, ninajua Yeye anahubiri kweli, maana hii hapa katika Biblia, ninajua hiyo ni kweli. Lakini sasa, kama umewaheshimu watu Wako kwa kutuma karama miongoni mwetu, basi, Bwana, jalia nipate faida zake. Ama kama—kama siuhitaji . . . "

175 Kama huhitaji uponyaji, sema, "Bwana, gusa mtu humu ndani anayeomba," sema hivyo. Kama huhitaji uponyaji, hebu mtu mwingine, kulikuwa na mikono michache iliyoinuliwa iliyohitaji uponyaji, sijui walikuwa ni akina nani, lakini kama huuhitaji, wewe—wewe—wewe mwombee mtu mwingine anayeuhitaji. Useme, "Ninajua mtu fulani hapa anayehitaji uponyaji. Jalia Roho Mtakatifu aseme na mtu huyo, amwite mtu huyo." Liamini tu namna hiyo, uone kitakachotukia.

176 Loo, huu si ni wakati mzuri sana? Hili hapa, haidhuru ninasema nini, kama Mungu hatimizi Neno Lake, Yeye si Mungu. Sasa, hakuna dini nyingine inayoweza kuchukua msimamo huo. Yesu wetu hajafa, Yeye alikufa, kweli, bali alifufuka tena, Yeye yu hai milele. Mungu aliye hai na ashukuriwe.

177 Hapa, ili mpate kujua, huyu hapa maskini mama mmoja ameketi papa hapa, simjui, sijawahi kumwona maishani mwangu. Lakini mwanamke huyo ana ugonjwa wa ngiri. Hiyo ni kweli, sivyo, mama? Mlikuwa na imani zaidi ya mlivyodhania mlikuwa nayo, sivyo? Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako, mama, huko juu kabisa ili watu waweze kuona. Hilo hapo. Aligusa nini? Yule nanii Mkuu . . . Niseme jambo lingine, mwanamke huyo hatoki hapa, anatoka mji mwingine, Ukiah. Kama utaamini kwa moyo wako wote (Hiyo ni kweli kabisa.), unaweza kwenda nyumbani ukaponywe, kwa kuwa Yesu Kristo anakuponya. Amina.

178 Aligusa nini? Mwulizeni endapo aliwahi kunijua? Sina njia ya kujua hilo. Lakini ilikuwa ni kitu gani? Angalieni *pale*, hivi hamwezi kuona ile Nuru ingali imening'inia juu ya mwanamke huyo papo *hapo*? Angalieni hiyo Nuru, papo *hapo*.

179 Kuna mama mwingine, anayerudi moja kwa moja nyuma yake pale, moja kwa moja nyuma hivi, anaugua ugonjwa wa kike. Bi. Haggy, utaamini kwa moyo wako wote kwamba Mungu . . .? Hiyo ni kweli, hivyo ndivyo ulivyo. Mimi ni mgeni kwako. Unaugua ugonjwa huo, uliyeketi hapo ukiomba. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako ili watu waone.

180 Huyo hapo. Aligusa nini? Aligusa upindo wa vazi Lake, si vazi langu, yuko umbali wa yadi thelathini kutoka kwangu, akagusa upindo wa vazi la Kuhani Mkuu. Mnampenda? Iweni na imani, mwaminini Mungu.

Mtu fulani katika sehemu hii aamini.

181 Hapa, huyu hapa mtu ameketi hapa akiniangalia. Mtu huyo ana roho ya giza juu yake, ana kifafa. Unaamini ya kwamba Mungu atakuponya, akupe afya? Unateseka kwa kuanguka, uh, kifafa. Unaamini Mungu atakuponya, na kukupa afya? Kama unaamini, inua mkono wako, useme "Ninaukubali." Nenda nyumbani, na ibilisi na akuache, wala asikusumbue tena, katika Jina la Yesu Kristo.

182 Hapa, ninamwona mwanamke mwingine, ameketi papa hapa nyuma. Anaugua ugonjwa wa kikoromeo. Anainamisha kichwa chake, alikuwa akiomba. Alikuwa akiomba, "Bwana Yesu, jalia aniite." Aligusa upindo wa vazi Lake. Ee Mungu, usimwache aukose, tafadhali usimwache. Jina lake ni Bibi Strait. Vema, amini Bibi Strait, na uende nyumbani ukapate afya. Unaamini kwa moyo wako wote? Unaamini? Simama kwa miguu yako, na ushuhudie ya kwamba unaamini ya kwamba Mungu atakuponya. Vema. Kama wewe ni mgeni kwangu, inua mkono wako. Vema. Lakini wewe si mgeni kwa Kristo.

183 Kama huyo si Bwana Yesu yeye yule, sijui ni nini. Amina.

Unaamini kwa moyo wako wote? "Kama unaweza kuamini!"

184 Ninamwona mama mmoja ameketi moja kwa moja kupitia huku, anaugua, ana mateso, amerukwa na akili, ni ugonjwa wa wasiwasi, ugonjwa wa akili. Loo, laiti huyu mwanamke angaliweza tu kulishika! Mungu, niambie yeye ni nani, tafadhali niambie. Jina lake ni Bibi Adams. Bibi Adams, amini kwa moyo wako wote, na Yesu Kristo atakuponya. Je, unaamini kwa moyo wako wote? Unakubali uponyaji wako? Usiogope, kama unaogopa, daima utakuwa katika hali hiyo; ni mateso ya kiakili. Lakini usiwe na shaka, amini kwa moyo wako wote. Utafanya hivyo? Basi simama kwa miguu yako, Bibi Adams, simama kwa miguu yako. Simama, papa hapa, na uponywe katika Jina la Yesu Kristo.

185 Ninamkemea ibilisi huyo anayekusumbua kujaribu kukuepusha na jambo hili! Ibilisi anakudanganya, utakuwa sawa. Nenda nyumbani, na uwe mzima sasa. Mungu akubariki. Amina. Haleluya!

186 Kuna mwanamume papo hapo nyuma yake hapo, ameketi mwishoni, anaugua ugonjwa wa moyo. Bwana, unaamini ya kwamba . . .? Je, una kadi ya maombi, bwana? Unaamini Mungu atakuponya? Una ugonjwa wa moyo. Uliponywa papo hapo, Yesu Kristo alikuponya, uligusa upindo wa vazi Lake, walikuwa wakikuombea. Amina.

187 Ninakupa changamoto kuliamini!

188 Hapa, huyu hapa mwanamke ameketi papa hapa—papa hapa chini namna hii, anaugua bawasiri. Ee Mungu, niambie, nijalie kujua. Bibi Hudenpough, simama kwa miguu yako, na ukubali uponyaji wako, na upate afya, katika Jina la Yesu Kristo.

189 Ninawapa changamoto wasikilizaji hawa kuunenea Mwamba! Unamwamini kwa moyo wako wote? Ni wangapi humu ndani wanaoamini mko katika hali ya kuweza kuzungumza Naye sasa? Vema. Je, mnaweza kusema Naye? Basi wekeaneni mikono, wekeaneni mikono. Jambo ndilo hilo, mjisahau tu, semeni na Mwamba. Wekeaneni mikono, ninaomba dua, Mungu awaponye.

190 Baba wa Mbinguni, ninakuomba, katika Jina la Yesu, mshushe Roho Mtakatifu, na jalia waseme na Mwamba, nao Mwamba utoe maji Yake ya uponyaji, na nguvu, na uweza, furaha, na upendo, na msamaha wa dhambi. Tujalie, Bwana, ninawakabidhi Kwako, katika Jina la Yesu Kristo.

191 Nena na Mwamba, nao Mwamba utaleta nguvu Zake za uponyaji. Unaamini ya kwamba unanena na Mwamba? Kila mtu kubali uponyaji wako sasa, simama kwa miguu yako, simama kwa miguu yako. Jambo ndilo hilo. Amina. Haleluya! Semeni na Mwamba.

Sasa, hebu na tuinue mikono yetu na kumsifu Mwamba. Haleluya! Mungu asifiwe.

192 Tunakushukuru, Bwana Yesu, kwa ajili ya nguvu Zako, uweza Wako wa yote. Wewe ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Tunaunenea Mwamba, nao Mwamba unatoa maji Yake. Yesu yeye yule, jana, leo, na hata milele, Maneno Yako hayawezi kushindwa kamwe. Watu hawa ni Wako, Bwana, wanakupenda, wanakusifu. Bwana, wajalie wenye dhambi kuja kwenye madhabahu ya toba. Tujalie, Baba, katika Jina la Bwana Yesu.

193 Sasa, ni wangapi wenu mnaomkubali? Inua mkono wako, useme, “Ninaamini Yeye yuko miongoni mwetu.” Inueni mikono yenu, msifuni. Msifuni! Msifuni! Ni tukufu jinsi gani! Ni ajabu jinsi gani!

194 Hakuna kitu kingine kinachoweza kufanywa. Sijui kitu kingine cha kufanya sasa, Tayari amekifanya. Hakuna haja ya kufanyiza mstari wa maombi, Mwamba tayari uko hapa, Mwamba tayari unanena. Haleluya! Mwaminini tu Mwamba, nao Mwamba utatoa maji Yake. Ninawakabidhi kwa Mwamba wa Miaka, katika Jina la Yesu Kristo, Mwana wa Mungu.

60-0723 Sema Na Mwamba Nao Utatoa Maji Yake
Lake County Fairgrounds
Lakeport, California Marekani

SWAHILI

©2025 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org